



## **TAARIFA KWA UMMA**

Kufuatia agizo la Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Kassim (MB) kuagiza Vyuo Vikuu na vya Kati nchini kufungwa kuanzia leo tarehe 18/03/2020 ili kuepusha kusambaa kwa virusi vya corona (COVID 19), Uongozi wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) unatangaza kufungwa rasmi kwa Chuo kwa muda wa siku thelathini (30) kuanzia leo tarehe 18/03/2020 kwa kampasi za Dar es Salaam, Mbeya, Singida, Mtwara, Mwanza na Kigoma. Hata hivyo taarifa zaidi zitaendelea kutolewa kupitia Tovuti ya TAASISI ([www.tia.ac.tz](http://www.tia.ac.tz)) na akaunti binafsi za wanafunzi kadiri miongozo mbalimbali ya Serikali itakavyokuwa inatolewa.

Wanafunzi wote wanaoishi kwenye hosteli za TAASISI wanatakiwa kuwa wameondoka chuoni ifikapo kesho Alhamisi tarehe 19/03/2020 na mabweni yote yatafungwa. Aidha, hakuna mwanafunzi ataruhusiwa kuingia kwenye eneo la Chuo kwa kipindi hicho.

Pia usajili wa wanafunzi wa *March intake* 2020) umesimamishwa kwa muda wa siku thelathini (30)

**IMETOLEWA NA**

LUCIANA S. HEMBE

**KAIMU AFISA MTENDAJI MKUU  
18 MACHI, 2020**